# SEHEMU YA 2: TAFSIRI

# MCHANGO WA MWALIMU J.K. NYERERE KATIKA TAFSIRI NA MAENDELEO YA LUGHA

*H.J.M. Mwansoko*.

**Ikisiri**

Kwa kuzingatia tafsiri mbili za J.K. Nyerere, Julius Kaizer (1963) na Mabepari wa Venus (1969), makala inaeleza: (i) kwa nini Mwalimu Nyerere alitafsiri maandishi ya Shakespeare, (ii) ufanisi wa tafsiri zake, na (iii) mchango wa tafsiri hizo. Makala inaonyesha kuwa tafsiri hizo zinazingatia mbinu za kisemantiki zaidi kuliko mbinu nyingine ingawa hapa na pale mbinu ya kimawasiliano inatumika pia. Makala inataja mchango wa tafsiri hizo kuwa ni kukuza fasihi ya Kiswahili, kukuza msamiati na kuwatia ari wafasiri wengine.

## 1.0 Utangulizi

Mojawapo ya dhima kuu za tafsiri – ule mchakato wa uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi) hadi lugha nyingine (lugha lengwa) (taz. Catford 1965:20; Mwansoko 1996:1) – ni kuwa daraja la kuunganishia jamii mbalimbali za watu wenye lugha na tamaduni zinazotofautiana. Katika makala hii tunajaribu kuonyesha jinsi mwasisi wa taifa la Tanzania na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu J.K. Nyerere, alivyotumia tafsiri kuutambulisha utamaduni wa kibwanyenye na kimwinyi wa Ulaya Magharibi (hususani Uingereza) kwa hadhira ya wasomi wa Kiswahili wa taifa lake na mataifa mengine kunakozungumzwa Kiswahili. Makala inaonyesha mchango wa Mwalimu Nyerere katika fani ya tafsiri na athari yake katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Data za msingi za makala zinatokana na upekuzi wa makini wa tafsiri mbili za Mwalimu Nyerere – *Juliasi Kaizari* (1963)[1] na *Mapebari wa Venisi* (1969) – za tamthiliya za mwandishi mashuhari wa kiingereza wa karne ya 16, William Shakespeare.

## 2.0 Sababu za kufasiri maandiko ya Shakespeare (na Plato)

Ingawa kwa mtazamo wa harakaharaka, kama anavyobaini Ruhumbika (1983a: 86-89), "Kwa Mtanzania ambaye kukuza Kiswahili ni sehemu ya juhudi yake ya kujikosha ukoloni na kuimarisha utaifa wake, kutafsiri fasihi za kigeni (ukizingatia jinsi fasihi ilivyo sehemu muhimu sana ya utamaduni wa watu), hasa kama ni zile za lugha za haohao watawala wetu wa jana, huwa ni kama kusaliti," Mwalimu Nyerere alikuwa na sababu za msingi kabisa zilizomfanya atafsiri tamthilia za Kiingereza za William Shakespeare.

Awali ya yote, tamthiliya za Shakespeare huchukuliwa kuwa ni miongoni mwa maandiko bora zaidi ya kisanii ulimwenguni. Mwanafalsafa wa siasa ya ujamaa, Karl Marx, aliwaona Shakespeare na Aeschylus kuwa ni wasanii wa tamthilia wenye kipaji kuliko wote tangu dunia kuumbwa (Ruhumbika 1983a: 87). Lugha ya Shakespeare, kama ilivyo kwa wanafasihi bora wote (k.m. Moliere, Racine na Corneille, kwa upande wa Kifaransa; Pushkin na Tolstoy, kwa lugha ya Kirusi; Goethe kwa Kijerumani, n.k.) ni yenye usanifu wa hali ya juu kabisa, inayoakisi kipeo cha usanifu na utajiri wa Kiingereza. Tafsiri ya matini za kifasihi za aina hii ni chachu na hazina kubwa ya ustawishaji wa lugha zinazoendelea.

Pili, maudhui ya tamthiliya za Shakespeare yana umuhimu mkubwa kwa taifa changa la Tanzania. Tamthilia za *Juliasi Kaizari* na *Mabepari wa Venisi* zinaonyesha na kulaani kwa uwezo mkubwa wa kisanii udhalimu na madhambi ya mfumo wa kinyonyaji na unyanyasaji wa kibepari. Jamii za kibepari zimeonyeshwa jinsi zinavyoabudu utajiri, zinavyopenda makuu, vyeo na utawala wa kidikteta, na jinsi zisivyojali utu na haki za binadamu. Mwalimu Nyerere, akiwa amedhamiria kujenga taifa la kidemokrasia na lenye kufuata itikadi ya ujamaa, inayotoa fursa sawa kwa wananchi wake wote, alitafsiri tamthilia hizi za Shakespeare ili kuonyesha kukerwa kwake na itikadi ya ubepari, na kuibua mtazamo huohuo hasi (dhidi ya ubepari) miongoni mwa wasomaji wa tafsiri zake. Kwa hakika kufasiri *The Merchant of Venice* kama *Mabepari wa Venisi* (na sio '*Bepari wa Venisi*', mathalani) kulilenga kusisitiza kuwa "wafanyabiashara" wote wa Venisi katika tamthilia husika walikuwa mabepari wanyonyaji, na wala sio Shailoki peke yake. (Taz. pia Lwaitama, mbioni). Ikumbukwe kwamba kutoakana na unyeti wa fasihi ya Shakespeare, wataalam wa tafsiri wa zama za umisionari na ukoloni hawakujishughulisha nayo kabisa.

Tatu, Mwalimu Nyerere, akiwa shabiki wa ushairi[2], alivutiwa kutafsiri tamthilia za Shakespeare kwa vile ziliandikwa kwa mtindo wa mashairi guni, yaani yale yasiyo na vina. Japo mashairi guni yanatofautiana sana na mashairi ya Kiswahili ya kawaida au ya kimapokeo, bado yalimpatia Mwalimu Nyerere burudiko la kutosha baada ya kuwa amechoshwa na kazi zake za kawaida. Katika Utangulizi wake wa tafsiri ya *Juliasi Kaizari* mwandishi anakiri: "Nia yangu ilikuwa kupata jambo la kufanya wakati kazi zangu za kawaida zilipokuwa zimenichosha sana na nataka kiburudisho". (uk.3, msisitizo wangu).

Aidha Mwalimu Nyerere alitafsiri maandiko ya Shakespeare kwa Kiswahili kwa vile hii ilikuwa fani yake. Yeye alikuwa mwalimu wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari na ndiye aliyeandaa muhtasari wa somo la Kiswahili wakati wa ukoloni wa Waingereza (miaka ya 1950) hadi muda mfupi baada ya uhuru kwa ushirikiano na walimu wenzake wa Kiswahili, kama vile Mwalimu Erasto Mang'enya.

## 3.0 Ufanisi wa tafsiri za Nyerere

Katika taaluma ya tafsiri matini za fasihi zilizobuniwa kwa makini, kama vile tamthilia, ushairi, riwaya na hadithi fupi, huainishwa kama matini elezi ambazo

huegemea zaidi kwa mwandishi. Mwandishi hutumia lugha kuelezea hisia zake bila kujali jinsi maelezo yatakavyopokelewa na hadhira. Matini za namna hii hufasiriwa kwa kutumia (zaidi) mbinu ya tafsiri ya kisemantiki (au ya wazi) ambayo kwayo mfasiri hufasiri kila kipashio au neno katika matini chanzi jinsi lilivyo kwa kufuata sarufi ya lugha lengwa. Yaani tafsiri ya kisemantiki aghalabu huwa na mshindilio wa taarifa (taz. Mwansoko 1996, sura ya 3 na 6).

Mwalimu Nyerere alizingatia vema misingi hii ya tafsiri katika tafsiri zake. Aliheshimu ruwaza ya kishairi ya matini chanzi zake na akairudufu kwenye matini lengwa kwa kadiri ilivyowezekana. Aidha mfasiri huyu alijitahidi kushughulikia takribani vipashio na maneno yote yaliyomo katika matini chanzi katika tafsiri zake. Tazama mfano ufuatao.

1. **Brutus**: Be patient till the last.
Romans, countrymen, and lovers! Hear me for
my cause; and be silent, that you may hear:
believe me for mine honour; and have respect
to mine honour, that you may believe: censure
me in your wisdom; and awake your senses,
that you may be the best judge. (uk. 732)

2. **Brutus:** Tulieni mpaka mwisho.
Warumi, wananchi na wapenzi! Nisikilizeni kwa kisa
changu, na nyamazeni ili muweze kusikia: nisadikini kwa
sababu ya heshima yangu, na istahini heshima yangu ili
muweze kuamini: nihukumuni katika busara yenu, na ziamsheni
akili zenu ili muweze kuwa mahakimu hodari. (uk.56).

Hata hivyo isidhaniwe kuwa Mwalimu Nyerere alitumia tafsiri ya kisemantiki tu katika kazi yake. Pale ambapo mahitajio ya hadhira lengwa na utamaduni na mazingira yake yalionekana kuwa muhimu zaidi, mfasiri alitumia tafsiri ya kimawasiliano (au huru). Aina hii ya tafsiri hueleza mawazo katika misingi ya lugha, utamaduni historia na mazingira yanayoeleweka kwa urahisi na kukubalika na wasomaji wa lugha lengwa. Angalia kwa mfano tafsiri zifuatazo:

3. **Antonius:** Friends, Romans, countrymen, lend me your ears.

(uk. 733)

4. **Antoni:** Rafiki zangu, Warumi, wananchi wenzangu, nisikilizeni. [Badala ya 'niazimeni masikio yenu']. (uk. 58) (kutoka *Juliasi Kaizari*).

5. **Caezar:** Nor heaven nor earth have been at peace to-night:
Thrice hath Calphurnia in her sleep cried out,
"Help, ho! They murder Caezar!" (pg. 727).

6. **Caezar:** Leo mbingu wala nchi haikuwa na amani: Mara tatu Calpurnia kalia usingizini, "Yala! Yala! Wanamwua Caezar!" (uk. 38).

[Kilio cha "Yala! Yala!" kimezingatia utamaduni wa Kiswahili]. (Kutoka *Juliasi Kaizari*).

Aidha, takribani methali na nahau zote zimetafsiriwa kwa kutumia tafsiri ya kimawasiliano. Mifano:

7. Fast bind, fast find – Mfunga imara hapati hasara.
8. All that glisters is not gold – Kila kitu king'aacho usidhani ni dhahabu.
9. Hanging and wiving goes by destiny – Kifo na mke, yambile, si kuchagua, ni tua. (Kutoka *Mabepari wa Venisi*).

Mintarafu kaida za sarufi ya Kiswahili, mfasiri alijitahidi sana kutumia maumbo ya Kiswahili sanifu kadiri ilivyowezekana. Mathalani, maneno mengi ya mkopo yalitoholewa kwa kupanguliwa mikururo yake ya konsonanti au kufungua silabi zake:

| | | |
|---|---|---|
| 10. Abraham | - | Iburahimu |
| Frankfort | - | Frankifuti |
| Lisbon | - | Liziboni |
| Tripolis | - | Tripoli |

Hata hivyo vilikuwepo vighairi vichache:

| | | |
|---|---|---|
| 11. Mexico | - | Mexico |
| Calphurnia | - | Calpurnia |

## 4.0 Mchango wa tafsiri za Mwalimu Nyerere katika maendeleo ya Kiswahili

Tafsiri za Mwalimu Nyerere zimekuwa na manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa manufaa hayo ni haya yafuatayo:

**(a) Kukuza fasihi ya Kiswahili**

Mchango huu umefafanuliwa vizuri na mwanafasihi mzalendo mashuhuri, Profesa Gabriel Ruhumbika:

> Faida kubwa hasa tutakayoipata kutoka kwenye tafsiri za vitabu vya waandishi mashuhuri wa lugha zilizoendelea zaidi, vilivyochaguliwa kwa busara [k.m. tamthilia za Shakespeare] imo katika kupanua kiwango cha fasihi yetu, kwa sababu maandishi haya mara nyingi yanawakilisha matokeo ya urithi wa vizazi kwa vizazi, na mara nyingine hata kwa zaidi ya karne. (Ruhumbika 1983 b: 262).

**(b) Kukuza msamiati**

Kama ilivyo kawaida, tafsiri za lugha za kigeni aghalabu huingiza katika lugha lengwa maneno ya kigeni 'yanayokopwa' pamoja na dhana zake kutoka lugha chanzi. Lugha ya Kiswahili haikukwepa athari hii kutokana na tafsiri za Mwalimu Nyerere. Mifano:

12. **filosofa** - philosopher (msamiati sanifu sasa ni 'mwanafalsafa')
13. **stokingi** - round hose (Kamusi ya Johnson (1939) inawakilisha `dhana hii kwa neo "stoki." TUKI (1990) imesanifisha msamiati 'stokingi'/'soksi ndefu')
14. **paithagorasi** - pythagoras.

Kwa baadhi ya dhana mpya mfasiri, Mwalimu Nyerere, alilazimika kuunda msamiati yeye mwenyewe, na hivyo kuchangia katika upanuzi wa msamiati wa Kiswahili, ama kuweka misingi ya upanuzi huo wa msamiati. Tazama mifano ifuatayo:

15. **Gaoler** -Mlinzi-jela (msamiati sanifu sasa ni 'askari jela'/ 'mlinzi wa gereza')
16. **triumvirs** - Wakuu watatu waliotawala kwa *sharika* baada ya kifo cha Juliasi Kaizari. (Mkazo wangu, nadhani sasa tungesema kwa usahihi zaidi kuwa ni "wakuu watatu waliotawala kwa ushirika …").

**(c) Kuwatia ari wafasiri wengine wazalendo**

Tafsiri za Mwalimu Nyerere zimewahamasisha wazalendo wengine wa Tanzania huru sio tu kufasiri fasihi bali pia maandiko mengine ya kitaalamu yenye manufaa kwa jamii yetu. Mathalani, mwanasiasa mashuhuri Paul Sozigwa, aliyefanya kazi kwa kushirikiana sana na Mwalimu Nyerere, alitafsiri kitabu cha fasihi cha *Song of Lawino* na cha sayansi ya uchumi, *The North-South Dialogue*.

## 5.0 Hitimisho

Ingawa Mwalimu Nyerere katika Utangulizi wake wa Juliasi Kaizari amekiri kuwa tafsiri yake si ya kitaalamu na hivyo huenda ikawa na upungufu wa hapa na pale, kauli hii yapaswa kuchukuliwa kuwa ni namna ya waandishi wengi waadilifu kujitolea kubeba makosa yao ya kisanii, hata kama ni machache ama hayapo kabisa. Ni namna ya wasanii kujishusha badala ya kujikweza wenyewe.

Hata hivyo hii haimaanishi kwamba tafsiri za mwalimu Nyerere ni sahihi kabisa tangu mwanzo hadi mwisho. La hasha. Kulingana na nadharia ya tafsiri hakuna tafsiri iliyo sawa kabisa na matini chanzi. Hii ni kwa sababu tofauti za kiisimu, kiutamaduni, kihistoria na kimazingira kati ya lugha hufanya iwe vigumu kufasiri mawazo ya lugha moja katika lugha nyingine bila kupoteza, kuptosha au kubadili maana. Kwa hali hii, hata tafsiri za Mwalimu Nyerere zina mapungufu madogomadogo kama vile mkanganyiko wa baadhi ya tafsiri[3] jambo ambalo ni la kawaida kwa tafsiri nyingi.

Pengine kilicho muhimu zaidi kwa wafasiri na waandishi wa vitabu vya Kiswahili ni changamoto iliyotolewa kwao na Hayati Mwalimu J.K. Nyerere katika Utangulizi wa *Juliasi Kaizari*:

> …. Ikiwa ubovu wa tafisiri hii utawaudhi mabingwa wa Kiswahili kiasi cha kutosha kuwafanya watunge vitabu vizuri zaidi, au kutoa tafsiri nzuri zaidi, hapana atakayefurahi kunizidi. Kadhalika nitafurahi sana ikiwa tafsiri hii itawasaidia wanafunzi wenzangu kuendelea kujifunza Kiswahili zaidi ili waweze kukisema na kukiandika kwa ufasaha zaidi. Kiswahili ni lugha tamu na pana sana. Lakini utamu wake na upana wake hauna budi utumiwe zaidi ndipo utakapoongezeka. (uk.6).

**Tanbihi:**

i. ‘Namshukuru sana Dkt. Y.P. Msanjila, Mchunguzi Mwandamizi wa Isimu, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kuisoma rasimu ya kwanza ya makala hii na kuitolea maoni ambayo yamesaidia sana kuiboresha.

ii. Katika kutayarisha makala hii nimetumia toleo la awali la tafsiri lililojulikana kama *Julius Caesar*. Ikumbukwe kuwa toleo la pili na lililodurusiwa la tafsiri

hii ndilo liliitwa *Juliasi Kaizari*. Aidha ni muhimu kuzingatia kuwa katika siku za mwisho za uhai wake Mwalimu Nyerere alijishughulisha sana na kazi ya kutafsiri. Alitafsiri Biblia kwa ushairi na tayari vijitabu vine vya tafsiri hiyo vimeshachapishwa. Aidha mwalimu keshasawidi tafsiri ya Plato ya *The Republic of Plato* ambayo bado haijachapishwa.

iii. Mwalimu Nyerere ameshachapisha mashairi yake katika magazeti, vitabu vya washairi wenzake na hata kuchapisha tenzi zake binafsi, kama vile utenzi wa Tanzania! Tanzania! (1995).

iv. Mfano wa tafsiri zinazokanganya ni huu ufuatao:

17. **Gratiano:** O, my Antonio, I do know of these,
That therefore are only reputed wise,
for saying nothing: who, I am very sure,
If they should speak, would almost damn those ears. (pg. 186)

18. **Gratiano:** Ee, Antonio wangu, najua baadhi yao
Wenye sifa ya busara kwa kutosema chochote;
Ingawa nina hakika, kwamba kama wangesema,
Karibu wangelaani masikizio ambayo
Kwa kuwasikia wao yangeta menzi majinga.
(uk. 4; msisitizo wantu)
(Kutoka *Mabepari wa Venisi*)

## MAREJEO


Catford, J.C. (1965), *A Linguistic Theory of Translation*, London: OUP.

Johnson, F. (1939), *A Standard Swahili-Englishi Dictionary*, Nairobi: OUP.

Mwansoko, H.J.M. (1996), *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*, Dar es Salaam: TUKI.

Nyerere, J.K. (1963); *Juliasi Kaizari*, Nairobi: OUP.

Nyerere, J.K. (1969); *Mabepari wa Venisi*, Dar es Salaam, OUP.

Ruhumbika, G. (1983a) "Tafsiri za Maandishi ya Kigeni katika Kiswahili", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili II, Uandishi na Uchapishaji*, Dar es Salaam, TUKI: 83 – 97.

Ruhumbika, G. (1983b); "Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili," katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III, Fasihi,* Dar es Salaam, TUKI: 253 – 266.

*The Complete Works of William Shakespeare*, London, The Hamlyn Publishing Group Limited, 1958.

TUKI (1981); Kamusi *ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam, OUP.

TUKI (1996); *English-Swahili Dictionary*, Dar es Salaam, TUKI.